

## Muhtasari wa kitabu cha Yereimia

Kufuatana na mfululizo wa matukio na wakati Haiwezekani kuweka kila unabii wa Yereimia katika enzi ya mfalme anayehusika kwa uhakika. Maneno haya yanahusika zaidi katika mafungu ishirini ya kwanza, ambapo ujumbe mmoja au mwingine unaweza kufaa aidha kwa enzi ya Yosia au ya Yehoyakimu. Lakini hata hivyo, msomaji akitaka kufuatia unabii na matukio ya wakati wa Yereimia kwa mfululizo fulani (akiacha nje unabii kuhusu mataifa ya kigeni katika mafungu ya 46-51), utaratibu wa mafungu unaofuata hapa unapendekezwa:

Enzi ya Yosia (640-609 k.K.)	Mafungu ya 1 -6
Enzi ya Yehoahazi (609 k.K.)	Fungu la 22 (mistari ya 10-12 tu)
Enzi ya Yehoyakimu (609-597 k.K.)	Mafungu ya 7-20, 25, 26, 22 (mistari 1-9,13-23), 23, 35, 36,45
Enzi ya Jehoyakini (597 k.K.)	Fungu la 22 (mistari 24-30)
Enzi ya Sedekia (597-587 k.K.)	Mafungu ya 24, 27-33, 21, 34, 37-39, 52:1-30
Baada ya kuanguka kwa Yerusalemu	Mafungu ya 40-44, 52:31-34

### Siku za mwisho wa Yuda

Yer52	k.K.	Matendo ya Wababeli	Wayuda kupelekwa kifungoni
	605	Kodi kwa Yerusalemu	Vijana wateule (Dan 1:1-4;2Fal 24:10-17)
mst. 28	597	Kutekwa Yerusalemu	Watu bora wote (2Fal 24:10-17)
mst. 29	587	Kubomolewa Yerusalemu	Wengi waliobaki (2Fal 25:1-17)
mst. 30	582	Kupora Yuda tena	waliobaki nchini (baada ya Yer41:17-18)
mst. 31	561	Yehoyakini afunguliwa	(matumaini ya kurudi (2Fal 25:27-30)